# MWANASHERIA

JARIDA LA AFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR

AGC ZANZIBAR | ATTORNEY-GENERAL'S CHAMBERS

# "HAKI NA WAJIBU"



SCAN ME

TOLEO LA 004 JULAI - DISEMBA 2025

Scan kusoma Jarida kielektroniki
www.agcz.go.tz

HALIUZWI

# SALAMU ZA MHE. MWANASHERIA MKUU



**NACHUKUA nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kwa mara nyengine tena kukamilisha Jarida letu la MWANASHERIA Toleo la Nne.**

Baada ya shukran hizo, kwa heshima kubwa tunawakaribisha Wasomaji wetu katika Toleo hili la Jarida la Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar.

Jarida hili ni jukwaa rasmi la kuwasilisha taarifa muhimu kuhusu maendeleo ya Afisi na hatua ilizopiga katika kutekeleza majukumu yake.

Itakumbukwa kuwa mara kwa mara Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amekuwa akisisitiza umuhimu wa Taasisi za Umma kutoa taarifa kuhusiana na shughuli zinazotekelezwa na Taasisi hizo, ili kueleza matokeo ya utekelezaji wake.

Jarida la MWANASHERIA ni miongoni mwa juhudi za kutekeleza agizo hilo ambapo Wasomaji wetu mtapata kufahamu kwa kina shughuli zinazotekelezwa na Afisi yetu pamoja na elimu juu ya mambo mbali mbali ya kisheria.

Kwa muhtasari, katika Toleo hili la Nne zipo habari zinazohusu uteuzi alioufanya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kuniteua tena na kuniapisha kuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar pamoja na habari ya Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Haroun Ali Suleiman kuipongeza Afisi yetu kwa kazi nzuri iliyofanya kwa kipindi cha Miaka Mitano.

Aidha, ipo habari inayohusu hafla ya kumuaga aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Kesi na Mashauri ya Madai, Bw. Ali Ali Hassan ambaye amestaafu utumishi wa umma. Habari ya zoezi la utoaji wa elimu ya sheria kwa makundi mbali mbali katika jamii ikiwemo wanafunzi wa skuli.

Habari nyengine inahusu zoezi la kukusanya maoni ya sheria ya Msaada wa Kisheria Nambari 13 ya mwaka 2018.

Katika ukurasa wa kutoka Mahkamani, pamoja na Afisi kushinda mashauri mengi ya madai, tumeona upo umuhimu wa kuliandikia Shauri kuhusu Sheria ya Mufti Mkuu Zanzibar Nambari 4 ya 2021 ambayo Mahkama Kuu imethibitisha kuwa ipo kisheria kama ambavyo Mawakili wa Afisi yetu walivyokuwa wanatetea Shauri hilo.

Kwa upande wa Makala za kitaalamu, zipo mbili ambazo zitawawezesha Wasomaji wetu kujua “historia ya Mabaraza ya Kutunga Sheria Zanzibar” pamoja na kufahamu uchaguzi na namna ya kuunda Serikali Zanzibar.

Hivyo, tutaendelea kutoa taarifa sahihi na za kina ambazo zitawezesha Wadau wetu kufuatilia kwa karibu mchango wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika maendeleo ya sekta ya Sheria ili kuchochea utawala wa demokrasia na maendeleo kwa Wananchi wote.

Tunathamini sana ushirikiano na maoni yenu, kwani ni chachu ya kuboresha huduma zetu na kuendeleza dhamira ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika kulinda maslahi ya Wananchi na Taifa kwa ujumla.

Kwa mara nyengine tena, tunawashukuru waandaaji wote wa habari, makala, pamoja na taarifa mbali mbali zilizojumuishwa kwenye Toleo hili, na tunawaombea afya njema, ili waendelee kutoa mchango wao katika matoleo yanayofuata.

Mwisho kabisa, tunakuombeni mutenge muda wa kusoma Toleo hili na msisite kutoa maoni, ushauri na mapendekezo yenu kwa lengo la kuliimarisha na kuja na matoleo mazuri zaidi siku zijazo.

**Dkt. Mwinyi Talib Haji,**
**Mwanasheria Mkuu,**
**Zanzibar.**



Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar,
13 Barabara ya Fumba,
71125 Mjini Magharibi
Zanzibar - Tanzania.

Simu : + 255 22 233455
barua pepe:
agcsmz@agcz.go.tz
www.agcz.go.tz

# TAHARIRI



**TUCHUKUE fursa hii kuwakaribisha Wasomaji wetu kwenye Toleo letu la Nne linaloandaliwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu ambayo kikatiba ina jukumu la msingi la kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala yote ya kisheria.**

Madhumuni makubwa ya kuchapishwa kwa Jarida hili ni kutoa elimu kwa umma, juu ya mambo mbalimbali yanayowakabili hasa yale yanayotokana na changamoto za kisheria.

Kwa mujibu wa kumbukumbu, Afisi hii ni miongoni mwa Afisi kongwe zilizokuwepo kabla ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 na imeendelea kuwepo muda wote kwa kipindi kisichopungua miaka Mia Moja (100).

Afisi katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha Miaka Mitano (2020-2025), imefanya mambo mengi kwa mafanikio makubwa, ikiwa ni pamoja na kuandaa Miswada 56, ambayo imepitishwa rasmi na Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuwa Sheria kamili, sambamba na kuandaa kanuni 58.

Hili ni jambo kubwa linalopaswa kupongezwa hasa ikizingatiwa kuwa Miswada hiyo iliyoandaliwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu na hatimaye kupitishwa kuwa Sheria, imeweza kutatua changamoto nyingi za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Hivyo, tunaamini Sheria hizo ambazo mwanzo ziliandaliwa kama Miswada na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, zimepunguza changamoto za Wananchi kulingana na mahitaji mbalimbali ya kisheria.

Jambo jengine la kupongezwa ambalo limetekelezwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika kipindi cha Miaka Mitano, ni hatua ya kuzikusanya Sheria zote za Zanzibar kuanzia mwaka 1909 hadi 2024 na kuziweka kwenye nakala laini (*soft copies*).

Hakuna asiyejua kuwa teknolojia imerahisisha mambo mengi, hivyo hatua ya Sheria hizo kuwa kwenye nakala laini maana yake, itairahisishia jamii kama watumiaji wakubwa wa sheria, watafiti na wanaofanya rejea kuzipata kwa wepesi.

Tunavyoamini kwa kipindi hiki kuendelea kuzihifadhi Sheria kwenye karatasi ni kinyume na wakati, lakini uhifadhi wa aina hiyo hauchukui muda mrefu sana ikilinganishwa na uhifadhi unaotumia mbinu za kisasa.

Jambo jengine la kupongezwa ni la ushauri na usimamizi wa mikataba. Afisi inajivunia kwenda na kasi ya Awamu ya Nane kwa kupitia na kutoa ushauri kwa jumla ya mikataba 3,802 kwa kipindi cha Miaka Mitano. Mikataba hiyo inahusu ununuzi wa bidhaa, huduma, ujenzi, ukodishaji ardhi na ushauri elekezi.

Afisi imetoa mchango mkubwa katika ushauri hasa katika masuala ya ujenzi ambayo kwa sasa miundombinu yote iliyopo Zanzibar ikiwemo barabara, skuli, hospitali na viwanja vya michezo, imefanywa chini ya ushauri wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Kwa tunavyofahamu, yapo mambo mengi Afisi hii imeyafanya katika kipindi cha Miaka Mitano na karibu yote ni muhimu kwa jamii. Hata hivyo, tuchukue fursa hii kuipongeza Afisi kwa mambo hayo makubwa iliyoyafanya kwa ajili ustawi wa Wananchi wa Zanzibar.

Tunategemea Miaka Mitano inayokuja Afisi hii itatekeleza mambo mengi na kwa ufanisi zaidi kwa maslahi ya Wananchi wote.

Wito kwa Wasomaji wa Jarida hili kwa ujumla waendelee kutoa ushirikiano kikamilifu kwa Serikali katika kutekeleza vyema majukumu yake na ahadi zake kwa wananchi.

Tunaiomba jamii iendelee kusoma Jarida hili tukiamini kuwa kuna elimu na maarifa mapya watakayoyapata na kuwasaidia katika maisha yao.

Bodi ya Wahariri licha ya kufanya kazi kubwa ya kukamilisha Toleo hili la Nne, itaendela na ari zaidi ya kuyafanyia kazi maoni na ushauri mnaoutoa ili kuyaimarisha zaidi matoleo mapya ya Jarida la MWANASHERIA.

Kwa wenye maoni, ushauri na mapendekezo tunaomba msisite kuyawasilisha kwetu kupitia Anuani za Afisi kwa lengo la kuliimarisha zaidi Jarida letu.

**Shaaban R. Abdalla,**
**Mwenyekiti wa Bodi ya Wahariri.**


**BODI YA WAHARIRI**

**Mwenyekiti:**
Shaaban R. Abdalla
(Naibu Mwanasheria Mkuu)

**Wajumbe:**
Dkt. Abdul-Nasser H. Hikmany
Mdungi M. Mdungi
Salim M. Abdalla
Asya M. Ahmed
Shufaa A. Khamis
Nakhla A. Massoud
Abeid M. Saleh
Hamisa M. Makame
Faki H. Mjaka

**Msanifu:**
Kombo Z. Kombo (mzubeir)
**Mshauri:**
Ramadhan M. Suleiman

# Dkt. Mwinyi amuapisha Mwanasheria Mkuu



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi (kushoto) akiwa pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji katika hafla ya kumuapisha kushika wadhifa huo, Ikulu Zanzibar. Katikati ni Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said.*

**NA MWANDISHI WETU**

**RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amemteua na kumuapisha Dkt. Mwinyi Talib Haji kuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.**

Hafla ya uapisho imefanyika, Ikulu, Zanzibar na kuhudhuriwa na Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Khamis Ramadhan Abdalla, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, viongozi mbalimbali wa Serikali, vyama vya siasa na dini.

Akizungumza na Jarida hili baada ya kuapishwa, Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji, alimshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kumuamini na kumteua kwa kipindi cha pili kushika wadhifa huo.

Alisema Rais ameonesha imani kubwa kumteua, hivyo ana deni kubwa la kutimiza majukumu aliyokabidhiwa.

Dkt. Mwinyi alimuahidi Mhe. Rais kuwa atachukua jitihada na kutumia uzoefu alionao katika kuhakikisha anatekeleza na kuyasimamia kikamilifu majukumu ya Afisi yake ikiwa ni pamoja na usimamizi wa kesi za madai na usimamizi wa mikataba.

“Kama taasisi tutasimamia maeneo hayo ili kuendana na kasi ya maendeleo ambayo tumeianza Miaka Mitano iliyopita ili miaka ijayo iwe na tija zaidi na Afisi ya Mwanasheria Mkuu iwe sehemu ya mafanikio hayo”, alibainisha Dkt. Mwinyi Talib.

Aidha, Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema wataangalia sheria ambazo zinaonekana kikwazo kama ambavyo walivyofanya Miaka Mitano iliyopita ili sheria hizo ziendelee kuakisi kasi ya maendeleo.

Dkt. Mwinyi aliahidi kufanya kazi kwa bidii akiwa kiongozi wa Afisi hiyo ili kufikia mafanikio ambayo Afisi imejipangia kwa maslahi ya Wananchi wa Zanzibar.

Kwa upande wake, Naibu Mwanasheria Mkuu wa

Zanzibar, Ndg. Shaaban Ramadhan Abdalla alimshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kumteua Dkt. Mwinyi Talib Haji kuwa Mwanasheria Mkuu kwa kipindi chengine.

Alisema uamuzi huo wa Rais umepokewa kwa furaha kubwa na wafanyakazi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kuzingatia kuwa Dkt. Mwinyi Talib, ameisaidia Afisi hiyo kujenga umoja na mashirikiano miongoni mwa wafanyakazi wote.

Naibu Shaaban alisema, jambo hilo limeiwezesha Afisi kuisadia Zanzibar katika maendeleo kwa kutekeleza vyema sera, mipango na mikakati ambayo inakwenda sambamba na utekelezaji wa sheria za Zanzibar.

Katika salamu za pongezi, Mwakilishi wa Jimbo la Malindi aliyewahi kuwa mtumishi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Mhe. Abdulghani Ismail Zubeir, alimshukuru Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji kwa kumlea vizuri na kumkuza kiutendaji.

"Mafanikio yangu yanatokana na malezi mazuri ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu amenilea vyema kiutendaji na namshkuru kwa kuniachia alama katika maisha yangu", Mhe. Abdulghani alisema.

Aidha, alimuomba Mwanasheria Mkuu kuendelea kumsaidia na kumshauri katika majukumu yake ili aweze kutimiza matakwa na matarajio ya Wananchi wa Jimbo la Malindi.

Mhe. Abdulghani aliwashukuru watendaji wote wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kipindi chote ambacho walifanya kazi pamoja na kuwaomba waendelee kushauriana na kusaidiana.





*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji (katikati) akiwa na Naibu Mwanasheria Mkuu Ndugu Shaaban Ramadhan Abdalla (kushoto), pamoja na Mkurugenzi wa Idara ya Mapitio na Utafiti wa Sheria, Dkt. Abdul-Nasser Hikmany, baada ya kuwasili Afisini kwake Mazizini muda mfupi baada ya kuapishwa.*

# Dkt. Haroun aimwagia pongezi Afisi ya Mwanasheria Mkuu

NA MWANDISHI WETU

**WAZIRI wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Haroun Ali Suleiman, ameipongeza Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa kazi nzuri iliyofanya kwa kipindi cha Miaka Mitano.**

Dkt. Haroun ambaye ameteuliwa kwa mara nyengine kuiongoza Wizara hiyo katika Serikali ya Awamu ya Nane, alitoa pongezi hizo wakati akipokea Ripoti ya Utendaji Kazi ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kipindi cha Miaka Mitano (2020-2025), hafla iliyofanyika Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Dkt. Haroun alisema Afisi hiyo inahitaji pongezi kwa sababu imechukua juhudi kupunguza migogoro (ardhi) baina ya taasisi za Serikali na Wananchi ambayo imekuwa moja ya changamoto kubwa.

Waziri huyo, alisema, watendaji wa Afisi hiyo wameonesha uzalendo kwa nchi, kuwajibika ipasavyo katika majukumu na nidhamu ya hali ya juu wanapokuwa kazini na nje ya majukumu yao.

"Katika kipindi hiki cha Miaka Mitano mmefanya kazi vizuri mno kiasi kwamba migogoro ya ardhi baina ya Serikali na wananchi, haipo au imepungua kwa kiasi kikubwa", alisema Waziri Haroun.

Kuhusu zoezi la kukusanya Sheria za Zanzibar kuanzia mwaka 1909 hadi mwaka 2024 na kuziweka katika nakala laini '*soft copies*', Waziri huyo alibainisha kuwa jambo hilo ni kubwa na halijawahi kufanyika.

Aidha, alisema mafanikio ya Afisi hiyo ni mafanikio kwa Serikali yote ya Mapinduzi ya Zanzibar na yamemsaidia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kutekeleza vyema majukumu yake.

Waziri Haroun aliwataka wafanyakazi wa taasisi hiyo waendelee kuwa wazalendo na kumuunga mkono kwa vitendo Rais wa Zanzibar na Serikali katika harakati zao za kazini na nje ya kazi.

Alisema kuwa majukumu yake aliyofanya kwa wepesi ikiwemo katika Baraza la Mapinduzi kutokana na msaada wa moja kwa moja alioupata kutoka kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Aidha, aliiomba Afisi ya Mwanasheria Mkuu kufanya kazi kwa karibu na Idara ya Msaada wa Kisheria ili kuhakikisha malengo ya Idara hiyo yanatimia kwa ufanisi.

Kwa upande wake, Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dkt. Mwinyi Talib Haji, alisema yeye na watumishi wa Afisi hiyo wanaona fahari kwa namna ambavyo Waziri Haroun amekuwa akiwaongoza katika majukumu yao.

Aidha, aimsifu Waziri Haroun kwa sifa yake ya ulezi kwa kipindi chote cha Miaka



*Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Haroun Ali Suleiman akizungumza baada ya kupokea Ripoti ya Utendaji Kazi ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kipindi cha Miaka Mitano (2020-2025), hafla ilifanyika Afisi ya Mwanasheria Mkuu.*



*Baadhi ya watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wakisikiliza nasaha za Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Haroun Ali Suleiman (hayupo pichani) baada ya Waziri huyo kupokea Ripoti ya Utendaji Kazi ya Afisi hiyo kwa kipindi cha Miaka Mitano (2020-2025).*



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji akitoa neno la shukrani baada ya Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Haroun Ali Suleiman, kupokea Ripoti ya utendaji kazi ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kipindi cha Miaka Mitano (2020-2025).*

Mitano, huku akiwaongoza vyema ili kuepuka kufanya makosa katika utendaji wao.


Dkt. Mwinyi alisema anajivunia nidhamu na weledi wa wafanyakazi wake huku akipongeza ushirikiano baina ya Afisi yake na Wizara, mambo ambayo yamechochea kwa kiasi kikubwa mafanikio hayo.

Akiwasilisha Ripoti hiyo ya utendaji kazi ya Afisi kwa kipindi cha Miaka Mitano kutoka mwaka 2020-2025, Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Shaaban Ramadhan Abdalla alisema Afisi kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali imeweza kuandaa Miswada 56 na hatimaye Miswada hiyo ilipitishwa na Baraza la Wawakilishi na kuwa Sheria.

Kuhusu Mikataba, Naibu Shaaban alisema, Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilitoa ushauri wa kisheria kwa jumla ya Mikataba 3,802 iliyohusu masuala ya ununuzi ya bidhaa, huduma, ujenzi, Kodi na ushauri elekezi.

Naibu Shaaban alisema, Afisi iliendelea kuiwakilisha Serikali kwenye mashauri ya Kesi za madai ambapo jumla ya kesi 75 zilifunguliwa mahkamani, kesi 20 Serikali ilishinda na kesi Moja Serikali ilikata Rufaa.

Afisi kwa Mwaka 2024-2025 ilifanya mapitio ya Sheria Saba (7) ambazo zilifanyiwa utafiti wa kina katika maeneo makhususi yaliyokusudiwa.



*Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Haroun Ali Suleiman (katikati) akiwa na watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu baada ya kupokea Ripoti ya Utendaji Kazi ya Afisi hiyo ya kipindi cha Miaka Mitano (2020-2025), hafla iliyofanyika Afisi ya Mwanasheria Mkuu.*

## Makala maalum

# Uchaguzi, namna ya kuunda Serikali Zanzibar

**NA HAMISA MMANGA**



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, akila kiapo cha Urais mbele ya Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Khamis Ramadhan Abdalla. Katikati ni Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said, hafla iliyofanyika Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar.*

**UCHAGUZI si jambo geni katika nchi yoyote ya kidemokrasia. Ni jambo la kushirikisha Wananchi katika kuendesha nchi yao, kinyume na nchi zinazofuata mifumo ya kidikteta au kifalme.**

Uchaguzi ni mfumo ulioletwa na Azimio la Haki za Binadamu la Kizazi cha Kwanza baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Azimio hilo limeweka Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binadamu juu ya Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966.

Azimio hilo limeeleza kwamba kila binadamu yupo huru katika kushiriki na kuendesha nchi yake. Hivyo, uchaguzi unashirikisha Wananchi katika kuendesha nchi yao.

Makala hii itajikita kuzungumzia uchaguzi wa Zanzibar baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 hadi kipindi cha sasa.

**UCHAGUZI MKUU BAADA YA MAPINDUZI YA 1964**

Zanzibar, baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 haikuwa ikifanya uchaguzi hadi hapo katika miaka ya 1980.

Kwa wakati huo, nchi ilikuwa ikiendeshwa na Baraza la Mapinduzi na mamlaka ya kutunga Sheria yalikuwa kwa Baraza la Mapinduzi ambalo liliongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Itakumbukwa kwamba mara baada ya Mapinduzi ya 1964, Serikali ilipitisha Sheria iliyojulikana; Sheria ya Uwezo wa Kutunga Sheria (*Legislative Powers Law*), ambayo kifungu cha 2 cha Sheria hiyo kilieleza kama ifuatavyo:

"*The power to make law for the Government of the People's Republic of Zanzibar is hereby vested in the President of the Republic acting by and with the advice and consent of Revolutionary Council*".

Ikimaanisha kwamba mamlaka ya kutunga sheria kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar itakuwa kwa Rais wa Jamhuri akifanya kazi kwa niaba na kushauriana na kupata ridhaa ya Baraza la Mapinduzi.

Hivyo, katika kipindi hicho, Baraza la Mapinduzi ndilo lililokuwa na mamlaka ya kutunga Sheria na wajumbe wa Baraza waliteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Hali hiyo iliendelea hadi mwaka 1979 ambapo Serikali ilianzisha Katiba ya Zanzibar ya 1979 iliyoweka misingi ya haki za binadamu na demokrasia.

Katiba ilitoa uhuru wa kuchagua na kuchaguliwa pamoja na haki ya kupiga kura. Katiba hiyo ilianzisha Tume ya Uchaguzi na ilipewa mamlaka ya kusimamia uchaguzi wa Rais pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Serikali pia ilitunga Sheria ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar Namba 3 ya 1980. Sheria hii iliweka utaratibu na mchakato wa uchaguzi wa Rais wa Zanzibar na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Kwa kuwa kipindi hicho kilikuwa kipindi cha mpito, ambapo Serikali iliazimia kuimarisha demokrasia nchini, Katiba ya Zanzibar ya 1979 ilifutwa na kutaarishwa Katiba mpya ya Zanzibar 1984 na ilienda sambamba na kufutwa kwa Sheria ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar ya 1980 na kuanzishwa Sheria ya Uchaguzi namba 11 ya 1984.

Kwa kuwa idadi na mahitaji

ya watu yanaongezeka, Serikali ililazimika kuimarisha na kuweka mazingira bora yatakayokwenda sambamba na ongezeko na mahitaji ya watu. Katika kuliendea hilo, Serikali ilifuta Sheria ya Uchaguzi Namba 11 ya 1984 na kutunga Sheria mpya ya Uchaguzi Namba 4 ya 2018.

Sheria hiyo mpya imetoa mamlaka kwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar kusimamia na kuratibu masuala yote ya Uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

Ifahamike kwamba Uchaguzi Mkuu wa mwaka uchaguzi na kupiga kura.

Kama ilivyoelezwa kabla ya mwaka 1980 hakukuwa na uchaguzi. Uchaguzi, kuanzia mwaka 1980 hadi 1990, ulikuwa uchaguzi wa Chama kimoja cha siasa.

Baada ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitisha azimio la kuwa na vyama vyingi vya siasa 1992, uchaguzi tokea mwaka 1995 unaendeshwa kwa demokrasia ya vyama vingi.

Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano inalazimika kufuata mfumo wa kidemokrasia wa vyama vingi vya siasa.

Sheria ya Tume ya Uchaguzi, Sheria ya Uchaguzi na Sheria ya Usajili ya vyama vya Siasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ni wa saba tokea Zanzibar ishiriki uchaguzi wa vyama vingi vya siasa kuanzia mwaka 1995.

**NAMNA YA KUUNDA SERIKALI BAADA YA UCHAGUZI**

Kama tunavyojua kwamba, Serikali za kidemokrasia zinajengwa na mihimili mikuu mitatu ya kuendesha Nchi.

Kifungu cha 5A cha Katiba



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, akikagua gwaride maalum lililoandaliwa na vikosi vya ulinzi, mara baada ya kuapishwa kushika wadhifa huo, katika hafla iliyofanyika Uwanja wa New Amaan Sports Complex.*

2025 ni uchaguzi ulioendeshwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984. Katiba hiyo imeweka ukomo wa uongozi wa Miaka Mitano kwa Rais, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

Mchakato wote unaratibiwa na Tume ya Uchaguzi kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya 2018 ambayo imeweka utaratibu wa kuendesha

Aidha, kifungu cha 5 cha Katiba ya Zanzibar, 1984 kimeeleza "Zanzibar itafuata mfumo wa Kidemokrasia wa Vyama Vingi vya Siasa wenye kuheshimu utawala wa sheria, haki za binaadamu, usawa, amani, haki na uadilifu".

Hivyo, Tume ya Uchaguzi katika kutekeleza kazi zake, inaratibu uchaguzi wa vyama vingi vya siasa kwa mujibu wa

ya Zanzibar, 1984 kimetambua mihimili hii kama ni mgawanyo wa madaraka wa kuendesha nchi ambayo ni mamlaka ya utendaji, mamlaka ya kutunga Sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Umma na mamlaka ya kutekeleza utoaji haki.

Katiba imefafanua kwamba mamlaka ya utendaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar,



*Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla akila kiapo kutumikia wadhifa wake huo kwa kipindi cha pili, katika hafla iliyofanyika Ikulu, Zanzibar.*

mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma ni Baraza la Wawakilishi na mamlaka ya kutekeleza utoaji haki ni Mahkama.

Katika mgawanyo huo, mamlaka mbili za kuendesha nchi ndizo mara zote zinaathiriwa moja kwa moja na Uchaguzi Mkuu. Nayo, ni ile mamlaka ya kiutendaji ambayo inahusiana na uchaguzi wa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na mamlaka ya kutunga sheria ambayo inahusiana na uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Serikali za mitaa kwa upande wa uchaguzi wa madiwani.

Mamlaka ya utekelezaji wa utoaji haki, ni muhimili wa kipekee uliopewa kinga kwa muhimili wenyewe pamoja na watendaji wake kutoingiliwa katika kutekeleza majukumu ya utoaji haki.

Mara baada ya Tume ya Uchaguzi kutangaza mshindi wa kiti cha Urais wa Zanzibar kwenye uchaguzi wa vyama vingi vya siasa, Rais mteule baada ya kula kiapo cha uaminifu anapaswa aunde

Serikali.

Serikali anayopaswa kuiunda kwa mujibu wa Katiba ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa kama inavyofafanuliwa katika Kifungu cha 9(3): Muundo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utakuwa wa Umoja wa Kitaifa na utendaji wa kazi zake utafanywa katika utaratibu utakaohakikisha kuendelezwa katika umoja nchini na lengo la kufikia demokrasia.

Muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa Zanzibar ulianza mwaka 2010 baada ya Serikali kupitisha Sheria ya Kura ya Maoni Namba 6 ya 2010.

Sheria ilitoa uhuru kwa Wananchi kupiga kura na kuamua muundo wa Serikali wanayoitaka na hatimaye kupata Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Muundo ambao baadhi ya nchi za Afrika kama vile Afrika ya Kusini wanautumia katika kuendesha nchi.

Sababu kuu ya kuanzisha kura ya maoni kwa Zanzibar ilikuwa ni kukabiliana na hali ya mpasuko wa kisiasa iliyokuwa ikiendelea katika visiwa vya vyetu vya Unguja na Pemba baada ya uchaguzi wa 1995 na 2000.

Ili kuondoa mpasuko huo, Serikali ilifanya maridhiano baina ya Chama ya Mapinduzi na Chama cha Wananchi Civic United Front (CUF). Maridhiano ya kwanza yalishindwa kutekelezwa na hatimaye muafaka wa pili ulifanyika. Muafaka huo ulipelekea kuanzisha Sheria ya Kura ya Maoni ya 2010 na baada ya Kura ya Maoni kukubalika ilipelekea kufanya Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ikiwemo Marekebisho ya Muundo wa Serikali.

Hivyo, ili kufuata masharti ya Katiba, baada ya Uchaguzi Mkuu kumalizika ni kuunda Serikali ambayo lazima iwe na Muundo wa Umoja wa Kitaifa.

Mchanganuo wa Serikali hiyo umefafanuliwa katika Sehemu ya Pili na ya Tatu ya Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Imekuwa ni utamaduni wa nchi nyingi za Jumuiya ya Madola, kabla ya kuunda Serikali Rais mara baada ya kuapishwa anamteua Mwanasheria Mkuu.

Umuhimu wa kumteua Mwanasheria Mkuu mwanzo ni kumuwezesha Rais kupata ushauri wa kisheria kabla hajatekeleza majukumu yake ikiwemo ya kufanya uteuzi wa viongozi mbalimbali wakati kuunda Serikali.

Katika kuunda Serikali, kama ilivyoelezwa huko juu, Rais ataunda Serikali kwa mihimili miwili ambayo mihimili hiyo iliathiriwa moja kwa moja na uchaguzi.

Hivyo, kwa kuanzia, Rais atateua viongozi katika muhimili wa kiutendaji ikiwa ni pamoja na Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais.

Kwa mujibu kifungu cha 39 cha Katiba ya Zanzibar 1984, kimemtaka Rais ndani ya siku saba mara baada ya kushika madaraka, yaani baada ya kula kiapo, atamteua Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais.

Kwa kuwa ilielezwa kuwa Muundo wa Serikali ni ya Umoja wa Kitaifa. Hivyo, Katiba imeweka sharti la mtu anaefaa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais lazima atoke kwenye Chama cha Upinzani kilichopata nafasi ya pili katika matokeo ya kura za uchaguzi wa Rais.

Iwapo chama kilichotokea nafasi ya pili kimepata chini ya asilimia kumi za kura zote za uchaguzi wa Rais au Rais hatokuwa na mpinzani, uteuzi wa Makamu wa Kwanza utafanywa kutoka chama cha upinzani kilichotokea nafasi ya pili kwa wingi wa viti vya majimbo katika Baraza la Wawakilishi.

Aidha, Rais atamteua Makamu wa Pili wa Rais kutokana na miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Katika muendelezo wa kuunda Serikali, Rais ataanzisha Wizara mbalimbali katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Baada ya kuanzisha Wizara ndani ya siku kumi na nne baada ya kumteua Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais, atateua Mawaziri kwa kushauriana na Makamu wote wawili.

Mawaziri watateuliwa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Uteuzi wao utazingatia uwiano wa viti vya majimbo kwa vyama vya siasa vilivyomo ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Muundo wa Serikali pia utakuwa na Baraza la Mapinduzi ambalo linajumuisha Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais na Mawaziri pamoja na wajumbe wengine ambao Rais ataona inafaa kuwateua.

Muundo wa Serikali unaweza kuwa na naibu mawaziri ingawa Katiba haijaweka ulazima wa uteuzi wa naibu mawaziri kama ulivyoweka ulazima kwa uteuzi wa mawaziri na kutoa muda maalum kwa Rais kufanya uteuzi wao.

Uteuzi wa naibu mawaziri unafanywa na Rais kwa kushauriana na Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais.

Katibu wa Baraza la Mapinduzi ni Kiongozi muhimu sana katika muhimili wa kiutendaji na anashika nafasi kuwa Katibu Mkuu Kiongozi na kuwa Kiongozi wa Utumishi wa Umma kwa Zanzibar.

Rais baada ya kuunda Baraza la Mapinduzi atamteua Katibu wa Baraza la Mapinduzi ambae atakuwa na dhamana ya Baraza la Mapinduzi, kupanga shughuli za mikutano na kuweka kumbukumbu za mikutano ya baraza na kufanya shughuli nyengine atakazopangiwa na Rais.

Katika kuhitimisha muundo wa Serikali kwa upande wa kiutendaji, Rais atawateua Makatibu Wakuu katika Afisi ya Rais, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais na katika wizara mbalimbali kama Rais anakavyoona inafaa. Katiba ya Zanzibar haikuweka ulazima wa kuteuliwa naibu makatibu wakuu wa wizara.

Kwa upande wa muhimili wa kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma, Rais ni sehemu ya Baraza la Wawakilishi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 63 cha Katiba kimeeleza Muundo wa Baraza la Wawakilishi utakuwa na sehemu mbili. Sehemu moja ni upande wa Rais na sehemu ya pili ni upande wa wawakilishi.

Katika sehemu ya Rais, Katiba imempa uwezo wa kuitisha Mkutano wa Baraza la Wawakilishi kama ni sharti la kuunda serikali mara baada ya uchaguzi.

Hivyo, kwa mujibu wa kifungu cha 90 na 91 cha Katiba ya Zanzibar, Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utaitishwa si zaidi ya siku 90 baada ya kuvunjwa kwa Baraza la Wawakilishi kupisha Uchaguzi Mkuu, Rais wa Zanzibar pekee amepewa uwezo wa kuitisha Baraza la Wawakilishi na kuendelea shughuli zake.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni mfumo wenye lengo la kupanua ushirikishwaji wa kuendesha nchi na kuwa na maamuzi ya pamoja baina ya vyama vingi vya siasa.

Mfumo huo umeleta maridhiano na manufaa katika jamii na kuonesha ukomavu wa demokrasia nchini.





# Afisi ya Mwanasheria Mkuu yashinda rufaa ya kesi ya kikatiba

## Iliyofunguliwa kupinga uwepo wa Afisi ya Mufti

**MAHKAMA Kuu ya Zanzibar imejiridhisha na kuthibitisha kwamba Sheria ya Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar Nambari 4 ya 2021 iliyoanzisha Ofisi ya Mufti Mkuu imekidhi masharti ya Katiba.**

Uamuzi huo wa Mahkama Kuu, ulitolewa Novemba 17, 2025 mbele ya Majaji watatu waliosikiliza Rufaa ya Maombi ya Kikatiba Nambari 1/2023 ya Masheikh 26 wakipinga uamuzi wa awali uliotolewa na Jaji wa Mahkama Kuu Zanzibar Mheshimiwa Ibrahim Mzee Ibrahim uliotokana na Maombi ya Kikatiba Nambari 4/2022 aliyesema kwamba Sheria ya Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar haijakiuka masharti ya Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Majaji watatu wa Mahkama Kuu Zanzibar waliosikiliza rufaa ya kesi hiyo ya kikatiba na kutoa uamuzi utakaoingia katika vitabu vya kumbukumbu vya Sheria Zanzibar ni Mheshimiwa Jaji Said Hassan Said, Mheshimiwa Jaji Salum Hassan Bakari na Mheshimiwa Jaji Haji Suleiman Khamis.

Aidha, Majaji Watatu hao, wakinukuu kesi mbali mbali na Mikataba ya Kimataifa, walisisitiza kuwa ni muhimu sana katika kesi ya aina kama hii kuzingatia kwa makini mkusanyiko, mnyambuliko na muingiliano wa historia ya watu wa Zanzibar ambao asilimia kubwa ni waislamu.

Vile vile, walisema tokea nyakati za ukoloni wa kisultani, Hifadhi ya Muingereza na baada ya Mapinduzi kulikuwepo taasisi za kidini zilizokubalika na tawala zote; kama Mahkama za Kadhi, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na mfumo wake wa kiutawala unazingatia utaratibu wa kikatiba.

Hoja zote zilizowasilishwa na Wakata Rufaani kupitia Mawakili Hassan Kornel Kijogoo na Abdalla Juma Mohammed hazikuwa na mvuto katika macho ya sheria na; baadhi ya ushahidi na hoja nyengine zilitupwa kwa sababu zilikuwa mpya na ziliwasilishwa katika hatua ya rufaa na wala hazikuibuliwa tokea hatua ya awali wakati kesi iliposikilizwa chini ya Jaji Ibrahim.

Miongoni mwa hoja zilizowasilishwa na Wakata Rufaani ni ile iliyopinga uamuzi wa Jaji Ibrahim kwa kudai sababu zilizotolewa zilikuwa dhaifu na zilijikita zaidi kihistoria kwamba Sheria ya Mufti ni muhimu kwa sababu asilimia 90 ya watu wa Zanzibar ni waislamu na hivyo basi lazima iwepo sheria ya kuwadhibiti.

Hata hivyo, Wakili wa Serikali Mkuu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Said Salim Said, aliipinga vikali hoja hiyo na kusema kwamba Jaji Ibrahim alitoa sababu za msingi na zilijitosheleza katika uamuzi wake uliozingatia kwa kina na umakini mkubwa Mikataba na Miongozo ya Sheria za Kimataifa.

Vile vile, Wakili huyo alisema Jaji Ibrahim alizingatia historia ya watu wa Zanzibar na madhumuni ya kutungwa Sheria ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na kufafanua kinaganaga msingi mkuu wa kutungwa Sheria hiyo ni; kuratibu na kusimamia mambo ya waislamu Zanzibar.

Aidha, Wakata Rufaani walipinga uamuzi wa Jaji Ibrahim kwa madai ya kushindwa kuzingatia lalamiko la kuwepo ubaguzi katika Ofisi ya Mufti Mkuu kinyume na Kifungu cha 12 (5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Ilielezwa aina ya ubaguzi uliopo katika Ofisi ya Mufti ni viongozi wa dini wa juu na watendaji wao wanafaidika na fedha za serikali ikiwemo kulipwa mishahara, posho, magari na samani wakati viongozi kutoka dini nyengine wanaofanana kwa wadhifa na hao waliopo katika Ofisi ya Mufti Mkuu, hawapati maslahi kama hayo.

Kuhusu hoja hii, Wakili wa Serikali Said aliipinga na kusema hapana viashiria vya ubaguzi vilivyojitokeza na alisema kungelitokea matatizo Zanzibar kama ingelikuwa hapana sheria ya kuratibu na kusimamia mambo ya waislamu ambao ni wengi zaidi Zanzibar.

Alisisitiza madhumuni ya Sheria ya Mufti ni kuratibu na kusimamia mambo ya waislamu na sio kuingilia kati au kubughudhi mambo ya waislamu.

Wakili wa Serikali alisisitiza kwamba shughuli na mambo ya waumini wa dini nyengine yanasimamiwa kupitia sheria nyengine zisizokuwa za kidini.

Aidha, alisema Sheria ya Ofisi ya Mufti Mkuu haikuleta athari yoyote kwa wafuasi wa dini nyengine na kama wangeliathirika wafuasi hao, basi angalau mmoja wao angeliunganishwa katika kesi hii. “Walalamikaji/ Wakata Rufaani wa kesi hii ni Waislamu tu”, alisema Wakili wa Serikali.

Katika hoja nyengine Wakata Rufaani walidai Jaji Ibrahim alishindwa kisheria kutambua Sheria ya Mufti Nambari 4 ya 2021 kwamba inakiuka Kifungu cha 19 (2) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinachozuia kuingiza shughuli na uendeshaji wa





mambo ya dini ndani ya shughuli za Mamlaka ya nchi.

Hata hivyo, Wakili wa Serikali alipinga hoja hii, kwa kukosa msingi wa sheria ukizingatia Jaji Ibrahim aliridhika kwamba Sheria ya Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar Nambari 4 ya 2021 ilifuata na kuheshimu masharti ya Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Aidha, Wakili wa Serikali alisema hapana amri yoyote iliyotolewa na Ofisi ya Mufti Mkuu iliyowapiga marufuku Wakata Rufaani kufuata dini ya chaguo lao isipokuwa wanatakiwa wanapofanya ibada zao; yanayofunguliwa Mahkamani.

Aidha, akizungumzia uwezekano wa Waomba Rufaa kwenda Mahkama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Mahkama ya Haki ya Afrika Mashariki (EACJ), Wakili wa Serikali Mkuu kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Said Salim Said ambae ndie aliesimamia Rufaa hiyo kwa upande wa Serikali alieleza kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 24 (3) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984, uamuzi huo uliotolewa na Mahkama Kuu Zanzibar mbele ya Majaji watatu utakuwa ni Wawili, Kumbukumbu Namba 09/2016, (Mbele ya Jopo la Monica K. Mugenyi, PJ; Audace Ngiye na Charles Nyachae, JJ) uliotolewa tarehe 29 Septemba, 2020 ambapo ilibainishwa wazi kuwa, kwa kuzingatia kuwa Zanzibar sio Nchi Shirikishi wala taasisi ya Jumuiya; hivyo Zanzibar wala maafisa wake (watu wake) hawana uwezo wa kufungua shauri mbele ya Mahakama hiyo.

Kwa uamuzi huo, imebainika wazi kuwa Mahkama ya Rufaa ya Kikatiba imeuthibitisha uamuzi wa Jaji Ibrahim Mzee Ibrahim kuwa ulikuwa



*Mkurugenzi Idara ya Usimamizi wa Kesi na Mashauri ya Madai (PSA), Salim Said Salim akiwapongeza Mawakili wa Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya punde baada ya kutoka katika Chumba cha Mahkama Kuu, huko Tunguu Zanzibar.*

basi wasikiuke haki za wengine zinazolindwa na Katiba.

Kukataliwa kwa hoja zote hizo kunaipa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar ushindi mkubwa na wa kihistoria katika kuendesha na kusimamia Mashauri ya Kikatiba wa mwisho na hautokatiwa rufaa katika Mahkama ya Rufaa ya Tanzania.

Vile vile, alirejea uamuzi wa Mahkama Kuu ya Zanzibar katika Kesi maarufu ya Rashid Salim Adiy na wenzake 39,999 dhidi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar na Wenzake sahihi kisheria, na kwamba Sheria ya Kuanzishwa Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar Nambari 4 ya 2021, haikinzani na Katiba ya Zanzibar ya 1984.

**Imeandikwa na Ali Uki,**
**Skuli ya Sheria Zanzibar,**
**Zanzibar.**

# MATUKIO KA



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji (kulia) akipokea tunzo ya pongezi kutoka kwa Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Ndg. Shaaban R. Abdalla iliyotolewa kwa niaba ya watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kuteuliwa tena kushika wadhifa huo.*



*Mkurugenzi wa Idara ya Mapitio na Utafiti wa Sheria, Dkt. Abd picha na baadhi ya wadau walioshiriki kikao cha kukusanya m Biashara na Vibali kilichofanyika katika ukumbi wa ZSSF, Kariak*



*Baadhi ya Watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar wakifuatilia nasaha zilizokuwa zikitolewa na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji (hayupo pichani) kuhusu umuhimu wa kutimiza majukumu yao kwa wakati.*



*Naibu Mrajis wa Mahkama Kuu Zanzibar Mh kukusanya maoni ya wadau kuhusu Sheria y kilichofanyika katika ukumbi wa ZURA, Maisara*




*Baadhi ya Watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar wakiwa katika hafla ya kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji kwa kuteuliwa tena kushika wadhifa huo. Hafla hiyo imefanyika afisini Mazizini, Zanzibar.*



*Mawakili wa Serikali kutoka Afisi y wakitembelea eneo lenye mgogoro wa Mkoa wa Kusini Unguja.*

# ATIKA PICHA



lul-Nasser Hikmany (katikati) akiwa katika
maoni juu ya Utafiti wa Eneo la Leseni za
koo, mjini Zanzibar.



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji (katikati waliokaa) akiwa na watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwenye hafla ya kumpongeza kwa kuteuliwa tena kushika wadhifa huo.*



*ne. Khamis Rashid akichangia katika kikao kazi cha a Msaada wa Kisheria Nambari 13 ya mwaka 2018, mjini, Zanzibar.*





*Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Ndg. Shaaban R. Abdalla kulia akimkabidhi Jarida la Afisi ya Mwanasheria Mkuu Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Bw. George Mandepo wakati wa kikao kazi baina ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kilichofanyika Mazizini, Zanzibar.*



*a Mwanasheria Mkuu (wa pili na watatu kulia), ardhi na kuwasikiliza wamiliki wa eneo hilo huko Paje,*



*Viongozi mbali mbali wakifuatilia hafla ya kuapishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dkt. Mwinyi Talib Haji, Ikulu, mjini Zanzibar.*

# Mwanasheria Mkuu: Tuige mazuri yanayoachwa na wastaafu



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji akizungumza katika hafla ya kumuaga Mkurugenzi mstaafu wa Idara ya Usimamizi wa Kesi na Mashauri ya Madai, Bw. Ali Ali Hassan iliyofanyika afisini Mazizini, Zanzibar.*

NA MWANDISHI WETU

**MWANASHERIA Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji amewashauri Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria kufuata nyayo za aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Kesi na Mashauri ya Madai, Bw. Ali Ali Hassan kwa kufanya kazi kwa bidii na kutanguliza mbele uzalendo.**

Mhe. Mwanasheria Mkuu alitoa ushauri huo katika hafla ya kumuaga Mkurugenzi huyo ambaye amestaafu Utumishi wa Umma, huko katika ukumbi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu uliopo Mazizini, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema, tangu kuajiriwa, Bw. Ali alikuwa mzalendo wa dhati kwa nchi yake na kwamba alitekeleza vyema majukumu yake kwa kutanguliza mbele maslahi ya nchi.

Dkt. Mwinyi alisema katika utumishi wake, alitekeleza kwa ufanisi kwenye kila jukumu alilopangiwa kuanzia usimamizi wa kesi na mashauri madai, sambamba na ushiriki katika Bodi mbali mbali.

Aidha, Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema Bw. Ali alikuwa kielelezo cha mtumishi mwenye subira kutokana na kukumbwa na changamoto nyingi za kazi na aliweza kukabiliana nazo vyema.

Akitoa salamu Mkurugenzi huyo mstaafu, alimshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kumuamini na kumteua katika nafasi ya ukurugenzi ambayo aliitumikia hadi kustaafu kwake.

Bw. Ali alitumia nafasi hiyo kuwashauri wafanyakazi kuwa wavumilivu katika kipindi chote cha utumishi wao hasa ikizingatiwa kuwa, kazini kuna changamoto nyingi.

Akielezea historia yake, Mkurugenzi huyo alifahamisha kuwa alitumikia Utumishi wa Umma kwa jumla ya miaka 40 katika taasisi tatu alizozifanyia kazi nchini.

Alibainisha kuwa, Idara ya Mahkama aliitumikia kwa miaka saba, Kamisheni ya Ardhi na Mazingira aliitumikia kwa miaka saba na Afisi ya Mwanasheria Mkuu aliitumikia kwa miaka 26.

Aidha, aliwashauri wafanyakazi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuzidisha mapenzi miongoni mwao, kwani kwa kufanya hivyo, kutachochea ufanisi wa kazi na kuyafikia malengo ya taasisi hiyo.

Alisema haipendezi wafanyakazi kudharauliana kwa aina yoyote kwa sababu anayedharauliwa leo, kesho anaweza kuwa mtu mwenye cheo kikubwa.

Awali, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Ndg. Shaaban Ramadhan Abdalla alimsifu Mkurugenzi huyo msataafu kutokana na bidii na



*Mkurugenzi mstaafu wa Idara ya Usimamizi wa Kesi na Mashauri ya Madai, Bw. Ali Ali Hassan akitoa neno la shukrani kwa watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu.*









*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji akimkabidhi zawadi Mkurugenzi mstaafu wa Idara ya Usimamizi wa Kesi na Mashauri ya Madai, Bw. Ali Ali Hassan. Kushoto ni Wakili wa Serikali Mkuu, Bi. Hamisa Mmanga katika hafla ya kumuaga Mkurugenzi huyo.*

nidhamu yake katika utumishi wa umma.

Aidha, alimuelezea kuwa ni mtu aliyejaaliwa maarifa makubwa na kipawa cha hali ya juu katika kuitetea Serikali kuhusu mashauri mbali mbali ya madai.

Naibu Mwanasheria Mkuu huyo, alisema, licha ya kuwa Bw. Ali amestaafu Utumishi wa Umma, Afisi ya Mwanasheria Mkuu itaendelea kupokea ushauri wake hususan katika mashauri ya madai yanayohusu migogoro ya ardhi, eneo ambalo amebobea.

Hafla ya kumuaga Mkurugenzi mstaafu Bw. Ali Ali Hassan iliambatana na utowaji wa zawadi mbali mbali ambazo alitunukiwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na watendaji.



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji (katikati) akiwa pamoja na watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika hafla ya kumuaga Mkurugenzi mstaafu wa Idara ya Usimamizi wa Kesi na Mashauri ya Madai, Bw. Ali Ali Hassan. Hafla hiyo ilifanyika afisini Mazizini, Zanzibar.*



Makala maalum

# Ifahamu historia ya mabaraza ya kutunga Sheria Zanzibar

NA ALI ALI HASSAN

**HISTORIA ya utungaji sheria Zanzibar ilianza tangu Sultan wa Oman alipoanzisha utawala wake hapa Zanzibar mnamo 1832, ambapo Zanzibar ilikuwa Makao Makuu ya Utawala huo.**

Sheria za Kiislam zilikuwa sheria za msingi za Zanzibar na mahkama zilianzishwa na kusimamiwa na Sultan mwenyewe. Sultan alitoa haki kwa Mabalozi wa Nchi za Nje kusimamia raia wa nchi zao.

Uingereza ilitumia Mamlaka ya ziada kwa kuanzisha Ubalozi uliokuwa na uwezo wa kushughulikia kesi za madai na jinai baina ya raia wa Kiengereza na malalamiko yaliyoletwa na raia wa Sultani dhidi ya raia wa Kiengereza na utaratibu huo uliendelea hadi 1861.

Mnamo Juni 14 mwaka 1890, Zanzibar ilikuwa Himaya ya Kiengereza na Waziri wa Kwanza wa Sultani wa Zanzibar akateuliwa kuwa Mwakilishi wa Uingereza.

Mwakilishi huyo alikuwa na dhamana ya Posta, Ofisi ya Kazi, Forodha, Bandari, hazina na Polisi. Madaraka ya Sultani yalikuwa yamepunguzwa na hakuwa na uwezo wa kumuondoa au kumuhamisha Afisa wa Kiengereza na hata mshahara wake ulipangwa na Mamlaka ya Uingereza.



*Zanzibar Order in Council 1897* - Amri hii ilikuja kuhalalisha kutumika kwa Sheria za India na Uingereza. Kwa Amri hii, sheria zifuatazo zilitumika Zanzibar:

*Indian Lunacy Act;*
*Indian Penal Code;*
*The Whipping Act;*
*Indian Succession Act;*
*Indian Divorce of Marriage;*
*Bombay Civil Court Act;*
*Indian Evidence Act; na*
*Indian Limitation Act;*

***Zanzibar Protectorate Council***

Baraza hili lilianzishwa Aprili 21 mwaka 1925 na lilikuwa Baraza la Kumshauri Sultan likiwa na wajumbe

wafuatao na halikuwa na Muafrika hata mmoja:

Sultani - Mwenyekiti;

British Resident - Makamu Mwenyekiti,

Mwanasheria Mkuu,

Katibu Mkuu Kiongozi,

Katibu wa Masuala ya Fedha na,


wajumbe wengine watatu wa Zanzibar mikononi mwa British Resident na kutaka kwamba Sultani asitunge sheria bila ushauri na ridhaa ya Baraza la Kutunga Sheria.

***Order in Council 1936***

Amri hii iliruhusu watu wa Zanzibar, kwa baadhi ya kesi kuomba rufaa British Court kulikuwa na Waarabu 3, Wahindi 2, Muingereza 1 na Muafrika 1. Muafrika wa mwanzo kuwemo katika Baraza hilo alikuwa Sheikh Ameir Tajo ambaye alibaki katika Baraza hilo hadi Mapinduzi ya mwaka 1964.

**Utungaji Sheria Baada** (*Legislative Powers Law 1964*, ambayo iliunda Baraza la Mapinduzi na kulipa uwezo wa kutunga Sheria. Kifungu cha 2 cha Sheria hiyo kilieleza kama ifuatavyo:

"*2. The power to make laws for the Government of the Peoples' Republic of Zanzibar is hereby vested in*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi (kushoto) akimsikiliza Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid kabla ya kuhutubia Baraza la 11 la Wawakilishi Zanzibar, kulia ni Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Khamis Ramadhan Abdalla.*

kuteuliwa.

***Order in Council 1926***

Amri hii iliwezesha kuanzishwa kwa Baraza la Kutunga Sheria na Baraza la Utawala. Kuundwa kwa vyombo hivi viwili kuliweka utawala wa Serikali ya of Appeal for Eastern Africa.

Baraza la mwanzo la Kutunga Sheria liliundwa likiwa na maafisa 8 na wajumbe 7 wasio maafisa na likiongozwa na Rais wa Baraza hilo.

Kati ya Wajumbe hao 7

**ya Mapinduzi**

Baraza la Mapinduzi (*The Zanzibar Revolutionary Council*)

Mara baada ya Mapinduzi 1964, Amri ya mwanzo kupitishwa ni Sheria ya Mamlaka ya Kutunga Sheria *the President of the Republic acting by and with the advice and Consent of the Revolutionary Council*".

Sheria iliyofuata baadae ni *Existing Law Decree No. 1/1964*, ambayo ilikuja kuhalalisha kutumika kwa

sheria za kabla ya Mapinduzi kwa sharti kwamba zisomwe na mabadiliko muhimu ya kimapinduzi ili ziwiane na hadhi ya Jamhuri.

Pamoja na kuruhusu Sheria za nyuma kutumika, Katiba ya Zanzibar ya 1963 ilipigwa marufuku kutumika. Kuanzia hapo Mamlaka ya Kutunga Sheria yalikuwa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Sheria hizi kama zile tulizozipokea kutoka nje zinaitwa "*Decrees*".

Mnamo Aprili 26 mwaka 1964, Tanganyika na Zanzibar ziliungana na kupatikana Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baadhi ya Mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yalianza kushughulikiwa kimuungano chini ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hivyo, baadhi ya sheria zilizokuwa zinatumika Zanzibar ziliathiriwa na muungano. Mambo hayo yameorodheshwa katika Jedweli la Kwanza la Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977.

**Baraza la Kwanza la Wawakilishi la Zanzibar**

Mnamo Oktoba 1979, Baraza la Mapinduzi lilipitisha Katiba ya Zanzibar ya 1979 ambayo pamoja na mambo mengine ilianzisha Baraza la Kutunga Sheria la Zanzibar likiwa na wajumbe 109. Kifungu cha 22 cha Katiba ya Zanzibar ya 1979 inasomeka kama ifuatavyoi:

"22(1) Bila kuathiri masharti mengine yaliyomo katika ibara hii, Baraza la Wawakilishi litakuwa na wajumbe wafuatao:-

Wajumbe wote wa Baraza la Mapinduzi isipokuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

Wabunge wote wa kuchaguliwa na Wilaya za Uchaguzi waliomo katika Bunge la Jamhuri ya Muungano kutoka Tanzania Visiwani;



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la M
Hussein Ali Mwinyi akitoa Hutuba ya ufunguzi w
Wawakilishi Zanzibar.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi (katikati waliokaa) akiwa pamoja na Wajun
baada ya Hutuba ya ufunguzi wa Baraza la 11 la Wawakilishi Zanzibar.




*apinduzi Mhe. Dkt.*
*wa Baraza la 11 la*



*mbe wa Baraza la Wawakilishi mara*

Wajumbe wawili wa kuchaguliwa kutoka kila Kamati ya Mapinduzi ya Wilaya waliochaguliwa na Kamati ya Mapinduzi ya Wilaya.

Wajumbe wawili wa kuchaguliwa kutoka kila Kamati yaMapinduzi ya Mkoa waliochaguliwa na Kamati ya Mapinduzi ya Mkoa;

Makatibu wote wa Mikoa ya Tanzania Visiwani kwa mujibu wa madaraka yao;

Wajumbe wawili wa kuchaguliwa na Halmashauri Kuu ya Mkoa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa kila Mkoa;

Wajumbe wawili wa Tanzania Visiwani kutoka katika kila Jumuiya inayoongozwa na Chama waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi;

Wajumbe wasiozidi kumi walioteuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar."

Baraza la Wawakilishi kwa Mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984

Katiba ya Zanzibar ya 1979 ilifutwa na kuazishwa kutunga Katiba mpya ya mwaka 1984. Pamoja na mambo mengine, Katiba hiyo ilibadilisha Muundo wa Baraza la Wawakilishi na wajumbe wake walikuwa kama ifuatavyo;

Wawakilishi wa kuteuliwa majimboni;

Wawakilishi 10 wa kuteuliwa na Rais.

Wajumbe wanawake wa kuteuliwa;

Wakuu wa mikoa, na

Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.

Muundo huo ulikuja kurekebishwa na Marekebisho ya 2010 ya Katiba ya Zanzibar kwa kuwaondoa Wakuu wa Mikoa, kuongeza idadi ya Wawakilishi wanawake kutoka ailimia 30 hadi 40 na kumfanya Spika mjumbe pale ambapo hakutokana na wajumbe wa kuchaguliwa.

# Mawakili wa Serikali waonya wanafunzi dhidi ya dawa za kulevya



*Watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wakiwa katika picha ya pamoja na wanafunzi wa Skuli ya Sekondari ya Mpendae Zanzibar, ikiwa ni mwendelezo wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kutoa elimu ya kisheria kwa makundi mbali mbali ya kijamii.*

**NA MWANDISHI WETU**

WAKILI wa Serikali Mkuu kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Dkt. Mahfoudha Masoud Ali, amesema matumizi ya dawa za kulevya huathiri afya na kwamba hakuna faida inayopatikana katika matumizi ya dawa hizo.

Dkt. Mahfoudha aliyasema hayo kwa nyakati tofauti alipokuwa akizungumza na wanafunzi wa Skuli ya Sekondari ya Kiembe Samaki, Mpendae na Skuli ya Biashara Zanzibar, ikiwa ni mwendelezo wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kutoa elimu ya sheria kwa makundi mbali mbali katika jamii.

Alisema vijana wengi wakiwemo baadhi ya wanafunzi wamekumbwa na janga la utumiaji wa dawa za kulevya. Aliwaasa kujiepusha ili kulinda afya zao.

Wakili Mahfoudha alionya matumizi ya dawa za kulevya husababisha matokeo mabaya kwa wanafunzi na hivyo kuuwa ndoto zao na za familia zao.

Alisema, kila mwanafunzi ana ndoto ya kuwa mtaalam katika fani itakayomuwezesha kuishi vyema lakini anapojiingiza katika matumizi ya madawa ya kulevya ni vigumu kufaulu mitihani na kuzifikia ndoto zake.

“Kila mmoja ana ndoto zake za kuwa mtaalamu fulani lakini mukijiingiza tu katika madawa ya kulevya mumeisha na ndoto zenu zimeishia hapo” alionya Dkt. Mahfoudha.

Kwa upande wake, Wakili wa Serikali Sumayya Awadh Hassan alisema mwanafunzi anapojiingiza katika matumizi ya madawa ya kulevya, uwezo wake wa kufikiri na kusoma hushuka na hivyo huambulia kufeli masomo na ndoto zake.

Naye Wakili wa Serikali Rahma Salum Fundi aliwataka wanafunzi hao kutojaribu kujiingiza katika matumizi ya madawa ya kulevya kwani ni vigumu mtu kuyaacha anapoyatumia.

Akitoa ufafanuzi wa athari za utumiaji wa madawa ya kulevya, mtaalam kutoka mamlaka ya kudhibiti na kupambana na madawa ya kulevya aliyeambatana na Mawakili hao, Ndugu Zakia Abass Ali alisema, madawa aina ya Shisha ambayo vijana wengi hutumia ikiwemo wanafunzi, yana athari mbaya kimwili na kiakili, hivyo zipo kila sababu za kuepukana nayo.

Alisema matumizi ya madawa ya kulevya huathiri ubongo, baadhi yake husababisha maradhi ya kifafa na megine husababisha ugonjwa wa saratani ya koo na mapafu.

Kuhusu mada ya udhalilishaji, Wakili wa Serikali Mussa Hamad Tajo alisema, tatizo la udhalilishaji pia limeshamiri katika jamii hivyo ipo haja ya kila mwanafunzi kujilinda mwenyewe na kuwalinda marafiki zao dhidi ya viashiria vyote vya udhalilishaji.

Wakitoa neno la shukran kwa niaba ya wanafunzi wenzao, Mwanafunzi Fahmi A.







*Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Ndg. Mussa Tajo akizungumza na wanafunzi wa Skuli ya Biashara Zanzibar, ikiwa ni mwendelezo wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kutoa elimu ya kisheria kwa makundi mbali mbali katika jamii.*

Abdallah na Thamrat S. Ali waliishukuru Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kuwapa elimu ambayo itawasaidia katika makuzi na maisha yao kwa ujumla.

Aidha walisema watafikiria namna ya kuanzisha Klabu ya Kupambana na Dawa za Kulevya skulini hasa ikizingatiwa kuwa, zipo klabu tofauti ikiwemo za Mazingira lakini hakuna Klabu ya Kupambana na Dawa za Kulevya.

Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar imekuwa ikitoa elimu ya kisheria kwa makundi mbali mbali Unguja na Pemba ili kuhakikisha Wananchi wanapata uelewa wa kutosha wa sheria na kuepuka kufanya makosa.



*Mwanafunzi Thamrat S. Ali wa Skuli ya Sekondari Kiembe Samaki akichangia Mada iliyowasilishwa na Mawakili wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya wakati Mawakili hao walipofika Skulini hapo kutoa elimu ya kisheria.*

# Afisi ya Mwanasheria Mkuu yaombwa kurudi kwa wadau

**NA MWANDISHI WETU**

AFISA Mdhamini Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Pemba, Halima Ali Khamis, ameitaka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, kurudi tena kwa wadau, baada ya kuchakata Maoni ya Sheria ya Msaada wa Kisheria Nambari 13 ya mwaka 2018.

Mdhamini huyo aliyasema hayo katika ukumbi wa Wizara ya Fedha na Mipango Pemba, wakati akifungua kikao kazi cha kukusanya Maoni ya Sheria hiyo.

Alisema itapendeza baada ya kukusanya maoni hayo Afisi ya Mwanasheria Mkuu kurudi kwa wadau, ili kuona maoni yao kwa kiasi gani yamezingatiwa.

“Niwaombe wenzetu wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu, mkumbuke kurudi kwa wadau baada ya kukusanya maoni, ili kabla haijapelekwa hatua nyingine, kwanza wajiridhishe'', alifafanua.

Katika hatua nyingine Afisa Mdhamini huyo, alisema, msingi wa usaidizi wa sheria utaendelea kuwa mwarobaini wa upatikanaji wa haki kwa Wananchi wasiokuwa na uwezo wa kifedha na uwelewa wa sheria.

Alieleza kuwa, mazingira ya upatikanaji wa msaada wa kisheria bila ya malipo yamesaidia Serikali kuimarisha utawala bora na Wananchi kujua misingi ya kudai haki zao.

“Msingi wa usaidizi wa sheria kwa wananchi, umekuwa sehemu ya kuimarisha utawala bora na tunajivunia kwa kazi kubwa iliyofanywa na Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria Zanzibar'', alieleza.

Aidha, aliwataka wadau wa kikao kazi hicho, kuwa huru kutoa maoni kwa maslahi ya taifa, hatua itakayowezesha kuwa na sheria rafiki kwa watoa msaada wa kisheria na wasimamizi wa haki jinai na madai.

Awali, Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Mbarouk Suleiman Othman, alisema Afisi imeamua kuifanyia mapitio sheria hiyo ili iendane na mazingira



*Afisa Mdhamini Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Pemba, Halima Ali Khamis akifungua kikao kazi cha kukusanya maoni ya Sheria ya Msaada wa Kisheria Nambari 13 ya mwaka 2018 kwa wadau, hafla hiyo ilifanyika katika ukumbi wa Wizara ya Fedha na Mipango Chake Chake Pemba. Kushoto ni Wakili wa Serikali Mkuu kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Mbarouk Suleiman Othman na kulia ni Wakili wa Serikali Safia Saleh Sultan.*

yaliopo.

Alisema tayari wamekusanya maoni kwa upande wa Unguja na kwa sasa wanafanya hivyo kwa upande wa Pemba.

Alisema, wamekuwa na utaratibu wa kuzipitia sheria kadhaa, ambapo kwa sasa miongoni mwa uwezekano wa kupatikana msaada wa kisheria kwa mashauri ya madai, ikiwa mtu ameishtaki serikali.

Alisema ni muhimu kuanzishwa kwa vituo vya msaada wa kisheria, ambapo sheria ya sasa haijaeleza kuvitambua vituo hivyo, jambo yasiingizwe kwenye makosa yanayopewa msaada wa kisheria.

Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar ambayo imeanzishwa chini ya Sheria Nambari 6 ya Mwaka 2013 ambapo miongoni mwa majukumu yake ni kuzifanyia



*Wadau wa Sheria kutoka Kisiwani Pemba walioshiriki kikao kazi cha kukusanya maoni ya Sheria ya Msaada wa Kisheria Nambari 13 ya mwaka 2018, wakifuatilia mapendekezo yaliyotolewa kuhusu Sheria hiyo na Wakili wa Serikali Sumayya Awadh Hassan (hayupo pichani). Hafla hiyo ilifanyika katika ukumbi wa Wizara ya Fedha na Mipango Chake Chake Pemba.*

hizo ni Sheria ya Msaada wa Kisheria Nambari 13 ya mwaka 2018.

Akiwasilisha mapendekezo ya Sheria hiyo, Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Sumayya Awadh Hassan alisema, wameona upo ambalo kama wadau watahisi lina umuhimu.

Naye Said Rashid Hassan, kutoka Shirika la Msaada wa Kisheria na Haki za Binaadamu Zanzibar 'ZALHO', alishauri kuwa, makosa ya dawa za kulevya na yanayofanana na hayo, marekebisho sheria mbali mbali ili kuendana na mazingira ya sasa.

Katika hafla hiyo, wadau mbalimbali walihudhuria pamoja na Wasaidizi wa Sheria, Polisi, Masheha na Wadau wa haki za binadamu.

# Kibonzo..


MHH! SERIKALI IMETUAHIDI AJIRA LAKI TATU NA HAMSINI SISI VIJANA ITAWEZEKANA KWELI?
HAKUNA LISILOWEZEKANA VIJANA CHANGAMKIENI FURSA, UWAJIBIKAJI NA MKIISHI KWA KUTII SHERIA AJIRA ZITAPATIKANA
MP
DENNIS 2025

# Nasaha za Mshairi

## SHAIRI: TARATIBU ZA KUMILIKI ARDHI NA KUTATUA MIGOGORO NA HAMAD ALI KOMBO (DKT. MSHIKO)

1 Naja leo jukwaani Kuwajuza wasojuwa
Kupitia Afisini Mkuu Mwanasheria
Migogoro Ardhini Na inavyotatuliwa
Migogoro ya ardhi Raia tuiepuke

2 Yazidi hata miteni Migogoro inongia
Inayongia nchini Ardhi kugombania
Mmiliki hasa nani Wanashindwa kutambuwa
Migogoro ya ardhi Raia tuiepuke

3 Kidogo mutabaini Nataka ielezea
Muitie akilini Nakazi kuifanyia
Kukikwepa kisirani Hapa Zanzibaria
Migogoro ya ardhi Raia tuiepuke

4 Mmiliki hasa nani Naanza kuwatajia
Ardhi uwe makini Usije ukavamia
Utaingia shimoni Kama hujazingatia
Migogoro ya ardhi Raia tuiepuke

5 Kununua kwa fulani Aula kukugaiya
Alomiliki zamani Tokea kuasisiwa
Huwezi ngia shidani Memiliki kisheria
Migogoro ya ardhi Raia tuiepuke

6 Kurithi toka wazazi Walokwisha tangulia
Walomiliki ardhi Taratibu kisheria
Hiyo yako wazi wazi Unaweza itumia
Migogoro ya ardhi Raia tuiepuke

7 Kukodi ni umiliki Nayo hii pia njia
Kwa njia ilo ya haki Kuendeleza wajuwa
Uwekezaji lukuki Kile ulotarajia
Migogoro ya ardhi Raia tuiepuke

8 Pori kwenda kulifyeka Lisilo la Serikali
Ambalo limeepuka Migogoro mbali mbali
Kulitumia mpaka Miaka kuminambili
Hilo ni lako hakika Taratibu ukizifata

9 Hizo njia umiliki Ambazo mewatajia
Hizo ni njia za haki Ikiwa utapitia
Migogoro haifiki Jamii ikaingia
Migogoro ya ardhi Raia tuiepuke

10 Njia zakuitatuwa Migogoro nawambia
Kusajili kisheria Aridhi hilo tambuwa
Hati miliki kupewa Toka wahusika juwa
Migogoro ya ardhi Raia tuiepuke

11 Kuweka yao mipaka Kusi Kaskazi pia
Mashariki na mpaka Magharibi ungekuwa
Urefu waelezeka Na upana lopangiwa
Migogoro ya ardhi Raia tuiepuke

12 Kurithi kwa uhalali Na hati ukapatiwa
Tena bila idhilali Taratibu kisheria
Kuepuka idhilali Zisijezikatokea
Migogoro ya ardhi Raia tuiepuke

13 Hizo njia mbali mbali Migogoro kutatuwa
Watufunua akili Afisi mwanasheria
Wanajitahidi kweli Elimu kutupatia
Migogoro ya ardhi Raia tuiepuke

14 Bora niweke kufuli Shairi namalizia
Limeshafika mahali Pale palokusudiwa
Kwani njia mbali mbali nimeshawaelezea
Migogoro ya ardhi Raia tuiepuke



AGC
ZANZIBAR
ATTORNEY-
GENERAL'S
CHAMBERS

# Attorney General's Chambers



SCAN ME

Fuatilia kurasa zetu za mitandao ya kijamii.

Afisi_ya_mwanasheriamkuu_znz